JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA

BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15

TOLEO LA BAJETI YA WANANCHI



Imetolewa na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Policy Forum

1 UTANGULIZI

Kijitabu cha Bajeti ya Serikali toleo la mwananchi kinatolewa kuboresha upatikanaji wa taarifa za kibajeti kwa lengo la kuongeza uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za umma. Kinaelezea bajeti ya Serikali kwa lugha rahisi, ikitoa dondoo za mambo muhimu kwenye bajeti na kuifanya kuwa rahisi kwa mtu wa kawaida kuielewa. Sera na mipango iliyomo katika bajeti ya Serikali huathiri maisha ya wananchi kwa namna tofaut itofauti, hivyo ni muhimu kwao kuitafakari kikamilifu maana yake.

Bajeti ya Serikali ni nini?

Bajeti ya Serikali ni chombo muhimu kinachotumiwa na Serikali kutekeleza maamuzi ya kisera ili kufikia malengo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hutoa makisio ya mapato na matumizi ya Serikali katika kwa mwaka husika. Msingi wa bajeti ya Serikali ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 137 (1) ambayo inaeleza kwamba, " Rais atatoa maagizo kwa watu wanaohusika kwamba, katika kila mwaka wa fedha wa Serikali, waandae na kuwasilisha kwenye bunge makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kipindi cha mwaka wa fedha unaofuata."

Bajeti ya mwaka 2014/15 imeandaliwa kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (Awamu ya pili), Malengo ya Maendeleo ya Milenia, Sera za kisekta, na Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2010 ya chama kilichopo madarakani; lengo likiwa ni kufikia Dira ya 2025.



2 SERIKALI INATAKA KUFANIKISHA NINI MWAKA 2013/14?

Mambo makuu ambayo bajeti ya mwaka 2014/2015 imelenga kuyafanikisha ni pamoja na: Kupunguza gharama za maisha kwa kuendelea na juhudi za kupunguza kiwango cha mfumuko wa bei; Kuboresha huduma za jamii; Kuboresha miundombinu ya barabara, nguvu za umeme na umwagiliaji maji; Kuboresha mishahara na tahili kwa watumishi wa umma; Kupunguza mzigo wa kodi kwa wafanyakazi; Kuongeza fursa za ajira na kuimarisha utawala bora; Haya yote yakiendana na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN)[1]. Bajeti pia imetoa umuhimu kwenye maandalizi yanaoendelea ya Katiba Mpya; Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2014; na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa 2015.

Madhumuni na Malengo ya kiuchumi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ni kama yafuatayo:

- ⇨ Pato halisi la Taifa linategemea kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2014 na kuendelea kukua kwa wastani wa asilimia 7.7.kwa kipindi cha Muda wa Kati;
- ⇨ Kuhakikisha kuwa kiwango cha mfumuko wa bei hakizidi tarakimu moja na kuendelea kushuka hadi asilimia 5.0 kufikia mwezi Juni 2015;
- ⇨ Kuhakikisha kuwa upungufu / nakisi ya bajeti haizidi asilimia 4.9 ya Pato la Taifa (GDP)[2] katika 2014/15;

[1] Matokeo Makubwa Sasa ni mpango wa Serikali unolenga kuweka mfumo imara na madhubuti wa kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mipango yake. Ni kuhusu kuwa na makubaliano ya vipaumbele vichache na kuhakikisha kwamba miradi iliyoibuliwa inapangiwa rasilimali ya kutosha ili itekelezwe kwa ufanisi.

[2] Pato la Taifa (GDP) ni kipimo cha jumla ya pato la utajiri ambalo linapatikana nchini kwa mwaka. Kwa maneno mengine, ni thamani ya bidhaa zote na huduma ambazo zinapatikana ndani ya nchi kwa mwaka.

- ⇨ Kudumisha ukuaji wa fedha kwa tafsiri pana (M3) katika kiwango cha asilimia 15.5 ifikapo mwezi June 2015, sambamba na ukuaji halisi wa Pato la Taifa na malengo ya kupunguza mfumuko wa bei;
- ⇨ Kuwa na akiba ya ya kutosha ya fedha za kigeni angalau kukidhi miezi minne (4) ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa mwaka 2014/15;
- ⇨ Kuimarisha thamani ya sarafu ya Tanzania kwa kudhibiti mwenendo wa soko la fedha za kigeni.

Ili kufanikisha malengo ya kiuchumi yaliyotajwa hapo juu, Serikali itatekeleza mambo yafuatayo:

- ⇨ Kuendelea kuboresha na kuendeleza amani na utulivu ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu;
- ⇨ Kuboresha na kuimarisha shughuli za kijamii na kiuchumi, biashara za nje na huduma za kifedha;
- ⇨ Kuongeza mapato ya ndani kwa: Kuimarisha vyanzo vya mapato vilivyopo, Kubaini vyanzo vipya vya mapato na kuongeza wigo wa kodi, na kupunguza misamaha ya kodi;
- ⇨ Kuimarisha mifumo wa usimamizi wa fedha pamoja na kuendeleza kudhibiti matumizi ya fedha za umma;
- ⇨ Serikali itanaboresha mfumo wa usimamizi wa fedha ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na uhakika wa upatikanaji wa fedha kabla ya kufanya ununuzi wa bidhaa au kutoa huduma;
- ⇨ Kuendelea kuunga mkono sera za fedha kuweza kupunguza shinikizo la mfumuko wa bei na pia kupunguza kupanda kwa viwango vya riba.
- ⇨ Kuendelea kuimarisha Utengamano wa Kikanda katika ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na ule wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kwa kutumia fursa zilizopo kikamilifu;
- ⇨ Kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuondoa vikwazo katika utekelezaji wa Sheria ya Ubia katika sekta ya umma na sekta binafsi, ili kuvutia ushiriki wa sekta binafsi katika ukuaji wa uchumi;
- ⇨ Kupunguza utoaji wa misamaha ya kodi na kubakia tu na ile ambayo inaleta tija kwa maendeleo ya uchumi; na
- ⇨ Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa bajeti ya Serikli kwa kuandaa Muswada wa Sheria ya Bajeti utakaowasilishwa bungeni kabla ya mwisho wa mwaka 2014/2015.

3 HATUA MUHIMU NA ZA KISERA KATIKA BAJETI YA MWAKA 2014/15

3.1 SERA ZA MAPATO:

Katika mwaka 2014/15, Serikali itaendelea na juhudi za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuchukua hatua mbalimbali za kisera na kiutawala.Hatua za kisera zitakazozingatiwa kwenye Bajeti ya mwaka 2014/15 ili kuongeza mapato ya ndani ni pamoja na:-

- ⇨ Kuimarisha mifumo ya kukusanya mapato pamoja na kuendelea kufanya mapitio ya sheria mbalimbali zinazotoa misamaha ya kodi kwa lengo la kudhibiti na kupunguza misamaha hiyo;
- ⇨ Kuongeza usajili wa walipa kodi wapya na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato;
- ⇨ Kuongeza siku za kufanya kazi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kutoa muda wa ziada wa kuwahudumia walipa kodi bandarini na baadhi ya vituo vya mipakani ;
- ⇨ Kukamilisha utungwaji na kuanza kutekeleza sheria mpya ya usimamizi wa Kodi;
- ⇨ Kuendelea kuimarisha na kusisitiza matumizi ya mashine za elektroniki za kutoa stakabadhi za kodi (EFDs) na kutoa elimu zaidi kwa walipa kodi na wafanya biashara kuhusu matumizi ya mashine hizo;
- ⇨ Kuwianisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi;
- ⇨ Kuongeza wigo wa kodi ikiwa ni pamoja na kuendelea kurasimisha sekta isiyo rasmi ili iingie kwenye mfumo rasmi wa kodi;
- ⇨ Wakala, Mamlaka za Serikali na Taasisi, zinazokusanya mapato yasiyo ya kodi, kuwasilisha maduhuli asilimia 10 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kupitia mfumo wa maduhuli;
- ⇨ Katika jitihada za kukabiliana na ukwepaji kodi, Wizara ya Fedha itatoa namba maalum ya simu na anwani ya barua pepe ili kuwawezesha raia wema kutoa taarifa mbalimbali kuhusu ukwepaji kodi; na
- ⇨ Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mikoa, Halmashauri, Wakala, Mamlaka na Taasisi zinazokusanya maduhuli na malipo mengine zinaagizwa kutumia mfumo wa kielektroniki ili kurahisisha ukusanyaji na kupunguza upotevu wa mapato.

Maboresho ya Mfumo wa Kodi, Ada, Tozo na Hatua nyingine za Mapato

Ili kuongeza mapato ya Serikali na kufikia malengo ya kiuchumi katika mwaka 2014/15, yatafanyika marekebisho ya baadhi ya mfumo wa kodi na tozo, ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi na tozo nyingine zisizo za kodi chini ya sheria mbali mbali kama ifuatavyo:

i. Kufanya marekebisho katika ***Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332*** ili Kutoa msamaha wa kodi kwenye mapato yanayotokana na mauzo ya Hatifungani zitakazotolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Hatua hii itawezesha Benki hiyo kuongeza uwezo wa kutoa mikopo nafuu ya uwekezaji kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo. Hatua nyingine ni kupunguza kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato ya ajira kutoka asilimia 13 hadi asilimia 12; Kuongeza kiwango cha kutozwa kodi kwenye mapato ghafi ya wafanyabiashara wadogo kutoka asilimia 2 hadi asilimia 4 kwa mauzo; na kuongeza kutoka shilingi 100,000 hadi shilingi 200,000 kwa wasiokuwa na kumbukumbu za mauzo;

ii. Kufanya marekebisho katika ***Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147*** ili kufuta Ushuru wa Bidhaa wa asilima 0.15 unaotozwa kwenye utumaji wa fedha. Badala yake kuweka ushuru wa asilimia kumi kwa Mabenki na Mawakala kwenye mapato wanayopata kwenye tozo na ada wanazokusanya kwenye shughuli za utumaji wa fedha. Marekebisho mengine yanajumuisha: Kuondoa msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwenye mafuta ya petroli; Kutoza ushuru wa asilimia 30 kwa magari ya umri wa zaidi ya miaka 10 na na asilimia 15 kwa yenye umri kati ya miaka 8 na 10. Pia kuongeza ushuru wa bidhaa kwa asilimia 20 kwa vitu

vinavyotengenezwa na tumbaku, na kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 15 kwenye samani zinazoagizwa kutoka nje ya nchi.

iii. Kufanya marekebisho ya ***Sheria ya Ushuru wa Mafuta, SURA 220***, ili kuondoa mamlaka ya Waziri wa Fedha kutoa msamaha wa Ushuru wa Mafuta, isipokuwa misamaha inayotolewa kwenye mikataba iliyosainiwa baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo.

iv. Kufanya marekebisho ya ***Sheria ya Ushuru wa Mauzo Nje, SURA 196***, ili kupunguza kiwango cha Ushuru wa Mauzo ya Nje kwenye ngozi ghafi zinazosafirishwa kwenda nje ya nchi Shilingi 900 kwa kilo moja hadi Shilingi 600 kwa kilo moja kutegemea kiwango kipi ni kikubwa.

v. Kufanya marekebisho ya ***Sheria ya Uwekezaji Tanzania, SURA 38;*** ili kurekebisha Mamlaka ya Waziri wa Fedha katika kutoa misamaha ya kodi ya uwekezaji.

vi. Kufanya marekebisho ya ***Sheria ya Leseni za Biashara Na. 25 ya Mwaka 1972***; ili kuipa Serikali mamlaka ya kutoza ada za leseni za biashara kwa viwango vilivyopendekezwa.

vii. Kufanya Marekebisho ya Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004; ili kuruhusu marekebisho ya viwango vya ushuru wa pamoja wa forodha kwa mwaka wa fedha wa 2014/15.

viii. Kufanya Marekebisho ya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na wizara, mikoa na idara zinazojitegemea ili kuvihuisha na kiwango cha sasa cha ukuaji wa uchumi.

ix. Usimamizi wa kodi zinazotozwa kwenye mafuta ya petroli yanapoingizwa nchini.

x. Kufanya marekebisho ya ***Sheria ya Fedha za Umma, SURA 348; Sheria ya Msajili wa Hazina SURA 418*** na ***Sheria ya Wakala wa Serikali SURA 245*** kwa minajili ya kuunganisha fedha zote za umma chini ya Mfuko Mkuu unaodhibitiwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.



3.2 SERA ZA MATUMIZI

Katika mwaka 2014/15, Serikali itatekeleza sera za matumizi zifuatazo:

- ⇨ Matumizi ya Serikali yatatakiwa kuendana na mapato;
- ⇨ Migao ya fedha katika taasisi za umma itatolewa endapo tu kutakuwa na uwasilishwaji wa taarifa za kila robo mwaka za utekelezaji wa mipango kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa;
- ⇨ Kuendelea kudhibiti matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na kuanzisha Sheria ya Bajeti;
- ⇨ Ili kupunguza gharama, Taasisi na Wakala wa Serikali zinatakiwa kutumia Wakala wa Serikali mtandao katika shughuli zote zinazohusu ufungaji wa mifumo ya kompyuta katika taasisi zao;
- ⇨ Ununuzi wote unaofanywa na Wizara, Wakala na Taasisi zote za Serikali lazima uambatane na matumizi sahihi ya mashine za ki elekroniki za utoaji wa risiti (EFD);
- ⇨ Malipo yote ya Serikali lazima yafanywe kupitia akaunti moja tu ya Serikali iliyoko Benki Kuu;
- ⇨ Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa nakisi ya Bajeti (ikiwa ni pamoja na misaada) isizidi asilimia 4.9 ya Pato la Taifa ;
- ⇨ Wizara, Mikoa, Halmashauri na Taasisi za Serikali zihakikishe kuwa matumizi katika mafungu yao hayavuki ukomo wa Bajeti uliopitishwa na Bunge.
- ⇨ Kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo;
- ⇨ Taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma kuwasilisha bajeti zao kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uchambuzi;
- ⇨ Uhakiki wa malipo kwa wakandarasi, wazabuni na malimbikizo/madai kwa wafanyakazi utafanywa na Wizara ya Fedha kwa kuzingatia mahitaji na bajeti ya Taasisi/Wizara/Mkoa husika;
- ⇨ Serikali kutekeleza mpango wa ununuzi wa pamoja kutoka kwa wazalishaji badala ya mfumo wa kununua kutoka kwa mawakala;
- ⇨ Kuendelea kutilia msisitizo kuzingatiwa kwa Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2004 na Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011;

4 FEDHA INATOKA WAPI NA NI KIASI GANI?

Katika mwaka wa fedha 2014/15 Serikali imepanga kukusanya jumla ya **shilingi bilioni 19,853.3** kutoka kwenye vyanzo vifuatavyo:

- ⇨ **Shilingi bilioni 12,178.0** zitatokana na mapato ya ndani (bila kujumuisha vyanzo vya Serikali za Mitaa), kati ya hizo, **shilingi bilioni 11,318.2** zitatokana na mapato ya kodi na **shilingi bilioni 859.8** zitatokana na mapato yasiyo ya kodi (*k.m.leseni na ada*).
- ⇨ **Shilingi bilioni 458.5** zitatokana na vyanzo vya Serikali za Mitaa (Halmashauri).
- ⇨ **Shilingi bilioni 922.2** zitatokana na mikopo na Misaada ya Kibajeti**.**
- ⇨ **Shilingi bilioni 2,019.4** zitatokana na Mikopo na Misaada ya Miradi ya maendeleo.
- ⇨ **Shilingi bilioni 2,955.2** zitatokana na mikopo ya ndani.

⇨ **Shilingi bilioni 1,320.0** zitatokana na Mikopo ya Nje yenye masharti ya kibiashara ili kugharimia miradi ya maendeleo.

Jumla ya Makusanyo ya Mapato ya Serikali na Vyanzo vyake



5 JINSI SERIKALI ILIVYOPANGA KUTUMIA FEDHA ZINAZOKUSANYWA

Jumla ya matumizi yaliyokadiriwa kwa mwaka wa fedha wa 2014/15 ni **shilingi bilioni 19,853.33.** Kiasi hiki kimeongezeka kwa asilimia 8.8 ukilinganisha na **shilingi bilioni 18,248.98** zilichokadiriwa kutumika mwaka 2013/14.

5.1 MGAWANYO WA MATUMI KATIAKA MAENEO MAKUU

i. ***Matumizi ya Kawaida*** (***Shilingi bilioni 13,408.22***): Hii ni jumla ya fedha ziliyopangwa na Serikali kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa Serikali. Ni gharama ambazo zitatumika kwa sehemu kubwa: (a) *Kulipia mishahara na marupurupu ya watumishi wa serikali*; (b) *Kununua bidhaa na kulipia huduma mbalimbali za Serikali* (kama vile vifaa vya shule, vifaa vya hospitali, mafuta ya magari ya Serikali, ukarabati majengo ya umma, kulipia pango la ofisi, n.k.); (c) *Kulipia madeni ya Serikali*. Kiasi kilichotengwa kwa matumizi ya kawaida kimeongezeka kwa asilimia 6.6 ukilinganisha na **shilingi bilioni 12, 574.95** zilizotengwa mwaka jana, 2013/14.

ii. ***Matumizi ya maendeleo (Shilingi bilioni 6,445.11):*** Hii ni jumla ya fedha zitakazotumika kugharimia miradi mbalimbali ya maendeleo kama vile: Ujenzi wa mashule na mahospitali; Usambazaji wa umeme na maji; Miradi ya kilimo; Ujenzi wa

miundombinu (k.m. mabarabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, n.k); Kusaidia maendeleo ya viwanda; n.k. Kiasi kilichotengwa kwa matumizi ya maendeleo kimeongezeka kwa asilimia 13.6 ukilinganisha na **shilingi bilioni 5,674.03** zilizotengwa mwaka jana, 2013/14.

Jinsi Fedha zilivyopangwa kutumika katika Maeneo Makuu.



5.2 MGAWANYO MATUMIZI KISEKTA

A: Sekta ya Elimu

Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Bajeti ya Sekta ya Elimu imeongezeka hadi kufikia **shilingi bilioni 3,465.1** kutoka **shilingi bilioni 3,127.9**, zilizotengwa mwaka 2013/2014. Hivyo, jumla ya shilingi **bilioni 337.2** zimeongezeka sawa na asilimia 10.8. Ongezeko la bajeti kwenye sekta linaonyesha ahadi ya Serikali ya kutekeleza miradi ya "Matokeo Makubwa Sasa" katika sekta ya elimu.

Vidokezo vya Mipango na Matumizi katika Sekta

Sekta ya Elimu imelenga kuboresha kiwango cha elimu na kuongeza fursa sawa kwa makundi yote, ikiwa ni pamoja na kundi la waliosahaulika (wanafunzi wenye ulemavu).Kufuatia vipaumbele hivi, mgao wa bajeti kwenye sekta ya elmu utaelekezwa katika nyanja zifuatazo:

i. *Elimu ya Mafunzo ya Ufundi na Ufundi Stadi*
   - ⇨ **Shilingi bilioni 13.4** zimetengwa kwa ajili ya kuviwezesha Vyuo vya Ufundi.
   - ⇨ **Shilingi bilioni 1.6** zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa Chuo cha Ufundi Arusha.

ii. *Elimu ya Msingi*
   - ⇨ Elimu ya Msingi imetengewa bajeti ya **shilingi bilioni 115.3** kwa ajili ya utawala na gharama za uendeshaji. Gharama za uendeshaji zinajumisha mitihani shilingi bilioni 26.2; capitation shilingi bilioni 29.9; likizo za walimu shilingi bilioni 12.0 na uhamisho shilingi bilioni 13.4.
   - ⇨ Ili kuboresha upatikanaji wa elimu kwa usawa katika ngazi zote kiasi cha **shilingi bilioni 9.7** kimetengwa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu wakiwemo watoto wa wafugaji na walemavu.

iii. *Elimu ya Sekondari*
   - ⇨ **Shilingi bilioni 92.3** zimetengwa kwa ajili ya gharama za uendeshaji. Gharama hizi ni pamoja na Mitihani **shilingi bilioni 14.9**; capitation **shilingi bilioni 19.9**; likizo za walimu **shilingi 4.6 bilioni** na chakula cha wanafunzi **shilingi bilioni 41.7**.
   - ⇨ **Shilingi bilioni 49.5** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa maabara, shule za sekondari 408 pamoja na vifaa vya maabara.
   - ⇨ **Shilingi bilioni 4.2** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Hosteli kwa wanafunzi wa Sekondari.

iv. *Elimu ya Juu*
   - ⇨ Ili kupanua elimu ya Juu, jumla ya **shilingi bilioni 247.3** zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kati ya hizo mishahara ni shilingi bilioni 215.8 na fedha za shughuli za utawala ni **shilingi bilioni 31.5**.
   - ⇨ Ili kuongeza upatikanaji wa mikopo kwenye Elimu ya Juu, jumla ya **shilingi bilioni 377.0** zimetengwa kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu.

- ⇨ **Shilingi bilioni 64** zimetengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Elimu ya Juu. Miradi iliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Muhimbili cha Afya na Tiba shilingi bilioni 2.4; Chuo Kikuu cha Ushirika na Biashara Moshi shilingi milioni 550; Ujenzi wa jengo la PMO katika Chuo Kikuu Mzumbe kwa gharama ya milioni 850 na shilingi bilioni 49 zimetengwa kwa ajili ya Mamlaka ya Elimu Tanzania.

v. Elimu ya Ualimu

- ⇨ **Shilingi bilioni 48.5** zimetengwa kwa ajili ya utawala na gharama za uendeshaji, ikijumuisha fedha za mishahara pamoja na matumizi mengineyo. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 shilingi bilioni 6.3 zimetengwa kwa ajili ya mafunzo ya ndani.
- ⇨ **Shilingi bilioni 13** zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa shule na vyuo.

B: Sekta ya Afya

Bajeti ya Sekta ya Afya kwa mwaka wa fedha 2014/15, ni **shilingi bilioni 1,588.2** ikiwa imepanda kwa asilimia 6 ikilinganishwa na **shilingi bilioni 1,498** zilizotengwa mwaka 2013/2014. Ongezeko la bajeti limelenga kuboresha huduma za afya ya kinga na tiba na hasa afya ya uzazi.

Vidokezo vya Mipango na Matumizi katika Sekta

Huduma ya Afya ni moja ya huduma muhimu kwa maisha ya mwanadamu katika nchi. Katika mwaka wa fedha 2014/15, kiasi kilichopangwa katika sekta kitatumika kuwezesha upatikanaji

wa huduma za afya kwa nchi nzima, katika namna ambayo itakuwa endelevu; kwa kuhakikisha huduma za kinga na tiba zilizo bora na za uhakika zinapatikana kwenye vituo vya huduma vilivyo karibu.

- **Shilingi bilioni 23.02** zimetengwa katika utoaji wa huduma bora ya afya ya Mama na Mtoto pamoja na kuzuia na kupunguza vifo vya Mama na Mtoto chini ya miaka mitano kwa kuendelea kugawa vidonge vya vitamini A na D kwa nchi nzima;
- **Shilingi bilioni 31.24** zimetengwa ili kuimarisha shughuli za afya ya msingi kwa wananchi kupitia Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi; katika ngazi ya wilaya, hasa katika ujenzi wa vituo vya afya, zahanati, ujenzi wa hospitali za wilaya. Kati ya hizo, shilingi bilioni 1.2 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa katika maeneo yaliyokuwa yamesahaulika na baadhi ya Halmasahuri;
- **Shilingi bilioni 15.94** zimetengwa kwa ajili ya kupambana na kuzuia UKIMWI na virusi vinavyosababisha UKIMWI kwa nchi nzima. Pia kutoa virusi vya UKIMWI;
- **Shilingi bilioni 278.1** zimetengwa kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa madawa, vifaa vya tiba na vitendanishi kwa ajili ya kuzuia na kutibu magonjwa ya kuambuiza na yasiyo ya kuambukiza. Kati ya hizo bilioni 134.90 zimetengwa kwa ajili ya UKIMWI na shilingi bilioni 35.72 kwa ajili ya malaria;
- **Shilingi bilioni 6.8** zimetengwa kwa ajili ya kusaidia huduma za afya kwenye Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI);
- **Shilingi bilioni 9.2** zimetengwa kwa ajili ya utoaji wa huduma za rufaa katika Hospitali yaTaifa ya Muhimbili;
- **Shilingi bilioni 260.3** zimetengwa kwa ajili ya uendeshaji wa huduma za Afya nchi nzima, kati ya hizo shilingi bilioni 116.63 kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa dawa muhimu na vifaa muhimu vya kitabibu kwa ajili ya kuboresha viwango vya huduma za afya ngazi ya wilaya na pia kuwajengea uwezo wahudumu wa afya katika ngazi ya Wilaya (madaktari,wauguzi na wakunga);
- **Shilingi bilioni 29.19** zimetengwa kwa ajili ya posho za madaktari kwa nchi nzima kwa ajili ya huduma za dharura, kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 7.13 kwa ajili ya madaktari wanafunzi;
- **Shilingi bilioni 3.0** zimetengwa kwa ajili ya Hospitali ya Saratani ya Ocean Road ili kutoa huduma za saratani ikiwa ni pamoja na ununuzi wa mashine ya mionzi;
- **Shilingi bilioni 26.5** imetengwa kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwenye Hospitali za rufaa nchi nzima, ikiwa ni pamoja na ununuzi na usambazaji wa madawa na vifaa vya tiba kupitia Bohari Kuu ya Madawa;
- **Shilingi bilioni 4.26** zimetengewa kwa ajili ya chakula, ujenzi wa madarasa, vyoo na uzio kwenye kambi za watoto na wazee wasiojiweza;
- **Shilingi bilioni 4.0** zimetengwa kwa ajili ya kupandisha hadhi hospitali za Wilaya kuwa za Mikoa katika mikoa mipya ya Simiyu,Njombe, Geita na Katavi;
- **Shilingi bilioni 3.5** zimetengwa jili ya ujenzi unaoendelea wa hospitali ya mkoa wa Singida;
- **Shilingi bilioni 0.45** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa hosteli za madaktari wanafunzi;
- **Shilingi bilioni 1.0** zimetengwa kwa ajili ya kupandisha hadhi hospitali ya Tumbi kuwa ya Mkoa.

C: Sekta ya Kilimo

Katika mwaka wa fedha 2014/15, Serikali imetenga bajeti ya **shilingi bilioni 1,084.7** kwa ajili ya Sekta ya Kilimo. Kiasi hiki ni ongezeko la asilimia 16.3 ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa mwaka 2013/14. Kiasi hiki kimeongezeka kutokana na umuhimu ambao Serikali imeipa sekta hususan katika utekelezaji wa Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa ya kilimo kwa kuwa kilimo ni sekta muhimu katika maendeleo ya nchi yetu kwa sababu inatoa ajira kwa asilimia 74 ya wananchi.

Vidokezo vya Mipango na Matumizi katika Sekta

Katika mwaka wa fedha 2014/15, sekta ya kilimo imepanga kutekeleza mikakati mahsusi ili kuweza kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo. Jitihada mbalimbali zinakusudiwa kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na: kuongeza ufanisi wa sekta ndogo ya ushirika, kuboresha huduma za ugani, pamoja na kuimarisha na kuboresha utoaji wa ruzuku kwa ajili ya pembejeo za kilimo kwa wakulima. Maeneo mengine ya kimkakati ni pamoja na kutengeneza mpango mkakati wa madawa ya kilimo, kutekeleza mikakati ya kuteketeza magonjwa sugu ya mimea na kuandaa rasimu ya sharia kwa ajili ya kulinda mashamba yaliyotengwa kwa ajili ya kilimo.

Mgawanyo wa fedha katika maeneo makuu utalenga katika shughuli zifuatazo;

- ⇨ **Shilingi bilioni 23** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya umwagiliaji katika halmashauri mbalimbali nchini;
- ⇨ **Shilingi 89.1** zimetengwa kwa ajili ya ruzuku ya kununua mbolea;

- ⇨ **Shilingi 6.3** bilioni kitatumika na Mfuko wa pembejeo kwa ajili kutoa mikopo ya pembejeo za kilimo zikiwamo Matrekta, mbegu, na jembe la kukokotwa na ng,ombe (Maksai);
- ⇨ **Shilingi bilioni 28.9** zimetengwa kwa ajili ya Tume ya Umwagiliaji. Fedha hizi zitatumika kufanya mambo mbalimbali yakiwemo utekelezaji wa miradi 39 ya umwagiliaji iliyo chini ya Ukanda wa Kilimo kusini mwa Tanzania (SAGCOT);
- ⇨ **Shilingi bilioni 111.3** zimetengwa kwa ajili ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ili kuwezesha kununua jumla ya tani 200,000 za nafaka kutoka katika maeneo yenye chakula cha ziada na kufanya ufuatiliaji ili kujua hali ya chakula nchini. Aidha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula itaanzisha kanda mpya katika Mkoa wa Kigoma itakayohudumia mikoa ya Kigoma, Geita, Kagera na Tabora. Wakala pia itajenga ghala la kuhifadhia nafaka lenye uwezo wa kuhifadhi tani 10,000 mjini Songea; na
- ⇨ **Shilingi 25.1bilioni** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la Kidunda kwa ajili ya kuimarisha umwagiliaji na udhibiti wa mafuriko.

D: Sekta ya Maji

Jumla ya **shilingi bilioni 665.1** zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kwa ajili sekta ya maji, kwa madhumuni ya kuboresha miundombinu ya maji mijini na viijini. Kiasi kilichotengwa ni kama asilimia 4.3 ya bajeti yote ya Serikali.

Dondoo za Mpango na Matumizi ya Sekta

Maeneo makuu ya Mpango na matumizi ni pamoja na ujenzi wa visima kwa kila Halmashauri; Ukamilishaji wa bomba la maji kutoka Ruvu Chini kupitia Bagamoyo hadi Dar es salaam; Usimamizi na uendelezaji wa vyanzo vya maji; Upanuzi wa mradi wa maji wa Ziwa Victoria-Shinyanga-Kahama kwenda wilaya za jirani za Nzega, Igunga na Tabora pamoja na vijiji na miji inayopitiwa na mradi; na Utekelezaji wa miradi inayoendelea pamoja na kuziwezesha Mamlaka za Miji za Maji kudhibiti upotevu wa maji na ukarabati wa miundombinu ya maji.

Hatua hizi pamoja na mambo mengine zinalenga kuondoa tatizo linalowakabili wananchi la kutembea muda mrefu kwa ajili ya kutafuta maji na kupoteza muda kwa ajili ya shughuli zingine za maendeleo; na pia kuondoa uwezekano wa watu kupata magonjwa yanayotokanayo na kutumia maji yasiyo salama.

Kazi Zifuatazo Zitajumuishwa Kwenye Mpango

- ⇨ **Shilingi bilioni 96.4** zimetengwa kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa miradi ya usambazaji maji vijijini.
- ⇨ **Shilingi bilioni 86.7** zimetengwa ili kutekeleza miradi ya usambazaji wa maji (miradi ya maji ya vijiji 10).
- ⇨ **Shilingi bilioni 148.2** zimetengwa chini ya Mikoa na Serikali za Mitaa ili kutekeleza miradi ya maji mjini na vijijini.
- ⇨ **Shilingi bilioni 50** zimetengwa ili kutekeleza miradi ya uchimaji visima na mabwawa ya maji.
- ⇨ **Shilingi bilioni 12.5** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji kwenye makau makuu ya mikoa.

- ⇨ **Shilingi bilioni 23.5** zimetengwa kwa ajili ya utekeleji wa mradi maalum wa kuboresha huduma za maji katika jiji la Dar es salaam.
- ⇨ **Shilingi bilioni 6** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji wa Kahama-Nzega-Tabora.
- ⇨ **Shilingi bilioni 15** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa usambazaji wa maji kutoka ziwa Victoria Shinyanga-Kahama.
- ⇨ **Shilingi bilioni 21.5** zimetengwa kwa ajili ya mradi wa bwawa la Kidunda.
- ⇨ **Shilingi bilioni 23** zimetengwa kwa ajili ya mradi wa maji wa Kimbiji na Mpera.
- ⇨ **Shilingi bilioni 30.3** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji wa Same-Mwanga-Korogwe.
- ⇨ **Shilingi bilioni 5.3** zimetengwa kwa ajili ya kampeni ya usafi na afya katika mashule, kaya, maonyesho ya wiki ya maji, vipeperushi na kwenye vyombo vya habari.

E: Sekta ya Usafirishaji

Katika mwaka wa fedha 2014/15 serikali imetenga shilingi bilioni 2,109 ukilinganisha na shilingi bilioni 2,139.02 zilizotengwa mwaka wa fedha 2013/14. Bajeti hii ni sawa na asilimia 14 ya bajeti yote ya serikali kwa mwaka 2014/15, tengeo hili limepungua kwa asilimia 1 ukilinganisha na bajeti iliyotengwa katika mwaka2013/14.

Serikali imeamua kuboresha barabara na sekta ya usafirishaji kwa kuchukua hatua mbalimbali, kati ya hatua hizo ikiwa ni kuihusisha sekta binafsi katika kugharamia miundombinu na kuiendesha shughuli za usfirishaji.

Aidha, Serikali imekusudia kukamilisha zoezi la kuunganisha mikoa na majiji yote nchini kwa lami, pamoja na kutengeneza mazingira mazuri ya sekta ya usafirishaji ili kuongeza chachu ya ukuaji wa uchumi na kuboresha huduma za kijamii nchini. Kadhalika serikali imekusudia kukarabati na kuboresha huduma za usafiri wa reli, usafiri wa anga na usafiri wa majini. Dondoo za mgawanyo wa fedha katika sekta hii ni kama ifuatavyo:

- ⇨ **Shilingi bilioni 126.9** zimetengwa kuimarisha na kuboresha utendaji wa Shirika la Reli –TRL (vifaa vya reli na ununuzi wa mabehewa);
- ⇨ **Shilingi bilioni 2.9** zitatumika kwa ajili ya treni ya abiria katika jiji la Dar es Salaam;
- ⇨ **Shilingi bilioni 261.6** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na uboreshaji wa viwanja mbalimbali vya ndege. Kati ya hizo, shilingi bilioni 44 zitatumika kwa ajili ya ujenzi/upanuzi wa Uwanja wa ndege wa Julius Nyerere (Terminal III);
- ⇨ **Shilingi bilioni 5.6** zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya vyombo vya usafiri wa anga, ununuzi wa rada ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, vifaa na miundombinu ya hali hewa;
- ⇨ **Shilingi bilioni 526.2** zimetengwa kwenye matumizi ya mfuko wa barabara kwa ajili ya matengenezo, ujenzi na usimamizi wa miradi mbalimbali ya barabara inayosimamiwa na TANROADS na Serikali za Mitaa;
- ⇨ **Shilingi bilioni 25.5** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa madaraja mbalimbali;
- ⇨ **Shilingi bilioni 7.4** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Kigamboni;
- ⇨ Ukarabati wa barabara za mikoa umetengewa shilingi **bilioni 31.9**;

- ⇨ Madaraja mbalimbali yakiwemo Kirumi, Nangoo,Sibiti,Maligisu,Kilombero na Lukuledi II yaemetengewa **shilingi bilioni 25.5** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya madaraja na ukarabati;
- ⇨ **Shilingi bilioni 28.9** zimetengwa ili kugharamia miradi ya uondoaji wa msongamano jijini Dar es salaam;
- ⇨ Mradi wa barabara ya Bagamoyo-Tegeta umetengewa **shilingi bilioni 14.5**;
- ⇨ Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga imetengewa **shilingi bilioni 10.2**;
- ⇨ **Shilingi bilioni 20.5** zimetengwa kwa ajili ya barabara ya Isaka- Lusahunga – Rusumo;
- ⇨ **Shilingi bilioni 36.6** zimetengwa kwa ajili ya barabara ya Kigoma – Kidawe- Uvinza-Kaliua mpaka Tabora.

F: Sekta ya Nishati na Madini

Bajeti ya Sekta ya Nishati na Madini kwa mwaka 2014/15 ni **shilingi bilioni 1,090.6** ikiwa ni pungufu kwa asilimia 2.0 ikilinganishwa na bajeti ya **shilingi bilioni 1,303.2** iliyotengwa mwaka 2013/14. Upungufu huu unatokana na kukamilika kwa baadhi ya miradi iliyokuwa ikitekelezwa mwaka 2013/14 ambapo miradi hiyo haijatengewa fedha kwenye bajeti ya 2014/15.

Mpango wa Matumizi katika Sekta

Sehemu kubwa ya vipaumbele vya Sekta ya Nishati na Madini katika mwaka 2014/15 ni mwendelezo wa vipaumbele vya 2013/14 kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na katika utaratibu wa Matokeo Makubwa Sasa. Vipaumbele hivyo vinajumuisha: Ufuaji, Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme; Ujenzi wa Miundombinu ya Gesi Asilia; Uhamasishaji wa uwekezaji kwenye Sekta ya Nishati na Madini; Uboreshaji wa makusanyo ya mapato katika Sekta ya Nishati Madini; na Kuimarisha uwezo wa usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya Sekta ya Nishati na Madini. Katika kutekeleza vipaumbele hivi, fedha zimetengwa kwenye miradi ifuatayo:

I. Ufuaji, Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme

- ⇨ **Shilingi bilioni 290.2** zimetengwa kutumiwa na Wakala wa Huduma ya Umeme Vijijini kwa ajili ya kusambaza umeme maeneo ya Vijijini na Makao Makuu ya Wilaya;
- ⇨ **Shilingi bilioni 145** kimetengwa kwa ajili ya mradi wa Mpango wa Ushirikiano wa Kitaasisi ili kuwezesha TANESCO kuimarisha uwezo wake katika kupanga na kusafirisha mfumo wa Umeme;
- ⇨ **Shilingi bilioni 90** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa mtambo wa kufua umeme kwa kutumia gesi wa MW 150 katika eneo la Kinyerezi - Dar Es Salaam, ili kuongeza umeme katika gridi ya taifa;
- ⇨ **Shilingi bilioni 5.0** zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu ya maji wa Hale, Tanga;
- ⇨ **Shilingi bilioni 22.5** zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha usambazaji wa umeme vijijini katika Wilaya za Ngara, Biharamulo na Mpanda;
- ⇨ **Shilingi bilioni 145.6** zimetengwa kwa ajili ya kuiwezesha Kampuni ya Umeme ya TANESCO kuongeza uwezo wa kufua, kusafirisha na kusambaza umeme kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na viwandani;
- ⇨ **Shilingi bilioni 50.3** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa KV 132 kutoka Makambako hadi Songea;
- ⇨ Bajeti ya **shilingi bilioni 11.8** ni kwa ajili ya uendelezaji na uhamasishaji wa matumizi ya nishati jadidifu; na

- ⇨ **Shilingi bilioni 4.0** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa mifumo ya usambazaji wa umeme.

II. *Maendeleo ya Gasi Asilia na Mafuta*

- ⇨ **Shilingi bilioni 117.0** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na mradi wa ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar Es Salaam;
- ⇨ **Shilingi bilioni 8.4** zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza Sekta ndogo ya Mafuta ili kuharakisha utafutaji wa mafuta nchini;

III. *Madini*

- ⇨ **Shilingi bilioni 13** zimetengwa kwa ajili ya umaliziaji wa ujenzi wa ofisi za madini za Mikoa ya Dodoma, Mpanda and Mtwara pamoja na uwekaji wa vifaa na samani kwenye ofisi za madini za Kanda;
- ⇨ **Shilingi bilioni 5** zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa mgodi wa makaa ya Mawe – Kiwira pamoja na ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme wa MW 200;
- ⇨ **Shilingi bilioni 3.2** zimetengwa kwa ajili ya uboreshaji wa Chuo cha Madini - Dodoma; na
- ⇨ **Shilingi bilioni 9.2** kimetengwa kwa ajili kuongeza uwezo wa Sekta katika usimamizi endelevu wa rasilimali za Madini.

G: Sekta ya Viwanda

Ili nchi iweze kufikia lengo la uchumi wa kati wa viwanda ifikapo mwaka 2025 iliyojiwekea kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 112.5 kwenye bajeti ya mwaka 2014/15, ikilinganishwa na shilingi 108.5 zilizotengwa mwaka 2013/14i. Kiasi hiki kimeongezeka kwa asilimia 3.67 ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa mwaka 2013/14. Maeneo yanayopewa umuhimu ni pamoja na uendelezaji wa kanda maalum za kiuchumi, kukuza uwekezaji wa viwanda vinavyoongeza thamani ya mazao ya kilimo, kuwezesha rahisisha na kuwezesha wajasiriamali wadogo na wakati kupata mitaji kwa urahisi.

Maeneo Makuu ya Matumizi

- ⇨ **Shilingi bilioni 7** zimetengwa kwa ajili ya kanda maalumu ya kiuchumi Bagamoyo (SEZ) ili kulipa fidia, kufanya uthamini na kuandaa makazi mapya kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi.
- ⇨ **Shilingi bilioni 53** zimetengwa kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Tanzania China Logistics Center-Kurasini, mbapo ukamilishaji wa kituo hicho utaongeza ajira ajira zaidi 25,000.
- ⇨ **Shilingi bilioni 5** zimetengwa kwa ajili ya miradi ya Mchuchuma na Liganga ambapo shilingi bilioni 2 zitatumia kwenye mradi wa Mchuchuma kwa ajili ya uthamini, mafunzo, upembuzi yakinifu, ujenzi wa miundombinu ya umeme na barabara; na shilingi bilioni 3 bilioni zitatumika kwenye mradi wa Liganga katika uthamini, fidia, ujenzi wa mgodi na ununuzi wa vifaa.
- ⇨ **Shilingi bilioni 2.03** zimetengwa kwa ajili ya kuanzisha soko la mazao na bidhaa, kuimarisha mfumo wa leseni za maghala na kuchangia utekelezaji wa miradi ya Programu ya ASDP inayolenga kuongeza thamani ya mazao ya kilimo.
- ⇨ **Shilingi bilioni 2.9** zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kuzalishia viatilifu vya kuua viluwiluwi wa mbu waenezao malaria mjini Kibaha.
- ⇨ **Shilingi milioni 990** zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa kituo cha umeme wa wa nguvu ya upepo Singida.

- **Shilingi milioni 804** zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha vituo 7 vya kuendeleza teknolojia vilivyoko chini ya SIDO, kutoa mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara kwa wajasiriamali wadogo na wa kati na kutunisha mtaji wa mfuko wa wafanyabiashara wananchi.
- **Shilingi bilioni 1.6** zimetengwa kwa ajili ya mradi wa "Rural Micro, Small & Medium Enterprise support programme" ili kusaidia upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwenye vikundi kama vile mbegu bora, madawa na mbolea, kutoa mafunzo ya kilimo bora na cha kisasa na kusaidia upatikanaji wa bei za mazao.
- Jumla ya **shilingi bilioni 1.2** zimetengwa kutekeleza mradi wa BEST ambao una lengo la kuandaa mfumo wa usajili wa makampuni kwa njia ya mtandao ambao utaraisisha usajili wa makampuni popote yalipo.

H: Kuongeza Ajira

Serikali imepanga kutekeleza Sera ya Kazi ya Taifa ya mwaka 2008. Lengo kubwa la sera ni kuongeza nafasi za kazi kwa kuandaa mazingira wezeshi kwa wadau wote kushiriki kikamilifu katika kuendeleza rasilimaliwatu. Katika kufanikisha lengo hili fedha zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2014/15 kama ifuatavyo:-

- Shilingi bilioni 3 zimetengwa ili kusimamia utekelezaji wa Programu ya Kukuza Ajira kwa Vijana ambayo imelenga kuwajengea vijana uwezo wa stadi mbalimbali za kazi na ujasiriamali; kuwapatia vijana mitaji yenye masharti nafuu na nyenzo za uzalishaji; na kutenga maeneo maalum ya uzalishaji, na maeneo ya kufanya biashara. Jumla ya ajira 700,000 zinategemewa kuzalishwa katika mwaka 2014/2015.
- Shilingi bilioni 230.7 zimetengwa ili kugharamia ajira mpya za watumishi 120,217 katika sekta ya Umma kwa mwaka 2014/2015 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 182.3 zilizotengwa kwa ajili ya watumishi 61,915 mwaka 2013/2014.



NYARAKA REJEA ZA BAJETI

Ifuatayo ni orodha ya nyaraka zinazochapishwa na Serikali na kutumika kama chanzo cha taarifa za kuandaa bajeti:

- Dira ya Maendeleo ya Tanzania, 2025 pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambayo imelenga ifikapo mwaka 2025 Watanzania watakuwa wameelimika vema na watakuwa wnaweza kujimudu wenyewe kiuchumi.
- MKUKUTA awamu ya pili, uonaanzia 2010 hadi 2015: Mkazo wake ni kutumia ukuaji wa uchumi kushushuglikia umaskini na mkazo mahususi ni juu ya jukumu la kilimo katika hili.
- Malengo ya Maendeleo ya Milenia, 2015: Mkazo ni kushughulikia njaa, elimu, usawa wa jinsi, afya ya mtoto na mama, kupambana na UKIMWI, mazingira endelevu, na kujenga ushirikiano wa kimataifa.
- Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala 2010 – 2015
- Mfumo wa Sera za Uchumi Jumla: Unatoa taarifa juu ya sera za bajeti na maboresho.
- Mkakati wa Taifa wa Madeni
- Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania
- Sera na Mikakati ya Kisekta
- Mfumo wa Tathmini ya Utendaji (PAF) chini ya Mapitio ya Mwaka ya Msaada wa Kibajeti (GBSAR)
- Hotuba za Bajeti za Mawaziri 2014/15
- Randama za Mipango ya Muda wa Kati na Mfumo wa Matumizi ya Muda wa Kati ya mwaka 2014/15
- Sheria ya Fedha ya Mwaka 2014
- Sheria ya Matumizi ya mwaka 2014
- Hotuba ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2014/15
- Tathmini ya Bajeti ya Serikali
- Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2014/15 (Juzuu Na. I –hadi IV)

Ili kupata baadhi ya nyaraka hizi na matoleo ya nyuma ya vijitabu vya Bajeti Toleo la Mwananchi, uneweza kutembelea mitandao ya:

- Wizara ya Fedha (www.mof.go.tz)
- Ofisi ya Rais – Tume ya Mipango (www.mipango.go.tz)
- Policy Forum (www.policyforum.or.tz)

Je, Utafanya nini na Taarifa hii?

Bajeti ya taifa ni taswira muhimu ya sura halisi ya kile ambacho Serikali inapanga kufanya kwa mwaka husika. Ukitaka kujua fedha yako ya kodi inakoenda, kama kuna mpango wa kuboresha elimu, afya, n.k katika eneo lako, unaweza kuangalia namna na jinsi ambavyo mgawanyo wa fedha unafanyika, hususan kwa ajili ya maendeleo. Kijitabu hiki kinajaribu kutoa muhtasari wa baadhi ya taarifa hizi kwa namna iliyo rahisi kadiri iwezekanavyo. Hata hivyo unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu mchakato wa uandaaji wa bajeti kutoka katika vyanzo vifuatavyo:

- Nyaraka zenye taarifa za bajeti ya Tanzania (***angalia orodha ya nyaraka za rejea***) na hasa, vitabu vinne vya bajeti ya taifa mbavyo vinapatikana katika Wizara ya Fedha (yaani Juzuu Na. I –hadi IV) .
- Wizara ya Fedha S.L.P 9111, Dar es Salaam (tovuti http://www.mof.go.tz)
- Ofisi za Halmashauri na/au Maofisa katika eneo lako kama Mwenyekiti Mtendaji wa Kijiji au
- Policy Forum, S.L.P. 38486, Dar es Salaam.

Kumbuka kwamba ni haki yako kujua bajeti hii na taarifa nyingine zinazohusiana na bajeti ya Taifa. Ongea na Viongozi wako kuhusu taarifa hizi na washirikishe watu wengine katika jamii unayoishi nayo.

…….……(Kwa maoni zaidi kata ukurasa huu)…….

Je, una mawazo gani, maswali, hisia (unafikiria nini), au una maoni gani kuhusu bajeti hii?

Je, unahitaji taarifa ziadi ya hii iliyotolewa katika kijitabu hiki? □NDIYO □HAPANA

Kama ndiyo Je, unahitaji taarifa ya aina gani?

Je kuna kitu kingine zaidi ambacho ungehitaji sisi tukijue?

Je, kijitabu hiki kilikusaidia? □ ndiyo □ hapana □ kiasi Fulani

Je kijitabu hiki kilikuwa rahisi kusoma na kueleweka? □ ndiyo □ hapana □ kiasi fulani

Tuma au fikisha sehemu hii

Wizara ya Fedha,
Idara ya Bajeti ya Serikali
S.L.P. 9111,
DAR ES SALAAM

Au tuma kwa njia ya barua pepe kwa: ps@mof.go.tz